Watumishi wa EWURA (toka kushoto) Bi. Radhia Ahmed, Ofisa mwandamizi wa Takwimu, Mhandisi James Mologosho, Mhandisi Mwandamizi wa Usambazaji Gesi Asilia, Mhandisi Godfrey Chibulunje, Mhandisi Mwandamizi wa Umeme, na Bi. Katrina Mshauri wa Mpango wa Maji EWURA akitokea taasisi ya GiZ ya Ujerumani.


HABARI KATIKA PICHA



Mkurugenzi wa Umeme wa EWURA, Mhandisi Anastas Mbawala (mwenye miwani) na Mkurugenzi wa Uchumi wa EWURA (aliyevaa T-shirt blu), wakijadili jambo na maofisa wa TANESCO, Wakurugenzi hao walipotembelea kituo cha kuzalisha umeme cha Kidatu hivi karibuni.



Watumishi wa EWURA, wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Bw. Haruna Masebu (mstari wa mbele kulia) na Meneja Rasidimili watu, B. Anna Clinton (mbele kushoto) wakishiriki kwenye mafunzo ya UKIMWI, Mitindo ya Maisha na Matayarisho ya Ustaafu, kwa ajili ya Watumishi wa EWURA yaliyofanyika Dar es Salaam Januari 2013.



Miundombinu ya Tanesco ya usambazaji wa umeme kwenye kituo cha kidatu, kampuni nyingi zaidi zinaomba leseni za kufua umeme.

Waomba leseni kuzalisha umeme wa megawati 150

Na Mwandishi wetu

Tanzania inatarajia kuongeza uzalishaji wa umeme kwa Megawati 150 ikiwa mipango ya kampuni mbili binafsi za kujenga mitambo ya kufua umeme katika mikoa ya Iringa na Ruvuma itafanikiwa.

Kampuni hizo, Kitunga Electric Power Company Limited na Tangulf Express Limited, tayari zimeionmba Mamlaka ya Udhambi wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA), leseni ya kujenga na kuendesha mitambo ya kuzalisha umeme.

Kitunga Electric Power Company Limited iliomba leseni ya kujenga na kuendesha mitambo ya kuzalisha umeme wa Megawati 150 kwa kutumia maji katika eneo la mto Lukosi wilayani Kilolo mkoani Iringa.

Kampuni hiyo imesema Megawati 140 za umeme utakaozalishwa

zitauzwa kwa TANESCO kwa utaratibu wa Mkataba wa Kuziana Umeme na Megawati 10 zitasambazwa katika vijiji vya Ukanda wa Image, yaani Image, Lyasa, Ibumu, Ikokoto, Mlifu, and Iyai. Kampuni ya pili Tangulf Express Limited iliwasilisha ombi la leseni ya kufunga mitambo,

Nyongeza hiyo ya umeme itasaidia upatikanaji zaidi wa umeme na kukuza uchumi.

kuendesha na kuzalisha umeme wa Megawati 9.2 kwa kutumia nguvu za maji toka mto Ruvuma katika Wilaya ya Songea, Mkoa wa Ruvuma. Umeme utakaozalishwa utauzwa kwa TANESCO kwa utaratibu uliowekwa chini ya Miradi Midogo ya Kuzalisha Umeme. Nyongeza hizo za umeme zitasaidia upatikanaji zaidi wa umeme na kukuza uchumi, hasa ikizingatiwa kuwa kumekwa na changamoto nyingi katika sekta ya nishati na upatikanaji wa umeme.

Hivi karibuni, shirika la kidini lilitalo African Benedictine Sisters of St. Agnes, nalo lililomba EWURA leseni ya kufunga na kuendesha mitambo wa kufua megawati 7.6 za umeme katika eneo la Tulla, mto Ruvuma, wilayani Mbinga, mkoa wa Ruvuma. Kiasi cha umeme huo kitauzwa TANESCO.

Tayari kampuni nyingine binafsi litwayo Mwenga Hydro Limited imeanza uzalishaji na usambazaji wa umeme wa Megawati nne wilayani Mufindi, Mkoani Iringa, hatua ambayo imeiwezesha TANESCO kununua karibu asilimia 80 ya umeme huo, na kiasi kinachobaki kinauzwa kwa kampuni ya Chai ya Mufindi.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Said Meck Sadik (katikati) akifungua Mkutano wa Taftishi wa Kujadili maombi ya TANESCO ya kurekebisha bei ya umeme , Disemba 2012. Mhe. Sadik alitoa wito kwa Watanzania kushiriki kwenye mikutano inayogusa maisha yao. Kulia ni mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Bw. Simon Sayore na kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu.



Jitokezeni kutoa maoni badala ya kulalamika - Mkuu wa Mkoa Dar

Na Mwandishi wetu

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Said Meck Sadik, amewapa changamoto Watanzania akiwataka kutumia mijiadala ya umma kuwasilisha maoni yao kuhusu masuala mbalimbali ambayo yatafikia uamuzi muhimu unaogusa maisha yao.

Kiongozi huyo alisema si haki kwa watu kukwepa majukwaa hayo, kama yale yanayoeendeshwa na Mamlaka ya Udhiditi

wa Nishati na Maji (EWURA) yanapotafutwa maoni ya umma juu ya masuala ya sekta kama vile ya umeme.

Bw. Sadick alikuwa akizungumza katika moja ya mijiadala hiyo iliyoendeshwa na EWURA Desemba 2012, jijini Dar es Salaam, katika mchakato wa kupitia viwango vya bei ya huduma za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Mapitio ya bei yanatokana na taarifa ya Utafiti wa Gharama za Huduma (COSS) uliofanywa na Mshauri Huru (AF MERCADOS EMI) wa Hispania.

“Nawaomba mtumie fursa kama hizo kutoa maoni yenu, yawe yanaunga mkono au yanapinga maombi ya malipo mapya yaliyowasilishwa na mtoa huduma wenu, msiache kujitokeza na kisha mlalamike umetolewa,” alisema.

Usikilizaji maoni ulijielekeza katika Maombi ya Kuongeza Bei ya huduma yaliyowasilishwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) likitaka yapande kwa asilimia 155.

Kwa kuzingatia Kitungu cha 15 cha Miongozo ya maombi

ya Bei ya mwaka 2009, EWURA kutokana na mapitio ya awali ya maombi hayo, ilitoa amri ambayo ilidhinisha ongezeko la dharura la bei ya umeme kwa asilimia 40.29. Bei hiyo ya dharura iliyoidhinishwa ilikuwa inadumu hadi Desemba 31, 2012.


Kwa mujibu wa utaratibu wa mchakato wa kukusanya maoni iliikwasanya maoni kutoka kwa wadau, ilikiwamo Baraza la Ushauri la Walaji (CCC), Baraza la Ushauri la Serikali (GCC) na umma kwa jumla.

Mkutano huo ambao ingawa ulihudhuriwa na watu wachache, ulikuwa na wachangiaji muhimu waliotoa changamoto nzito ambazo ndizo zilizodhinishwa maoni ya umma. Mwananchi wa kawaida wa Temke, Bw. Othman Omar Othman alilikosoa TANESCO kwa alichokita ni ukosefu wa “akili ya kibiasara”, akisema kampuni hiyo inashindwa kukusanya madeni kutokana na urasimu.

“Kampuni inadai kwamba nina deni la Sh 400,000...lakini hataki deni hilo lilipwe kwa awamu ... na sina uwezo wa kulilipa kwa pamoja ... hii ni biasara ya aina gani mnayofanya?” Alilalamika Othman.

TANESCO, alisema Othman, inahitaji malipo ya juu ili kuisaidia uwezo wa kukidhi malipo makubwa yanayokabili kutoka kampuni binafsi za kutua umeme kama vile Symbion, Agreko na IPTL. Matuta aghali ya kuendeshea baadhi ya mitambo mikubwa kama ya IPTL ni sababu nyingine ya bei kubwa ya huduma hiyo.

“Nawaomba mtumie fursa kama hizo kutoa maoni yenu, yawe yanaunga mkono au yanapinga maombi ya malipo mapya yaliyowasilishwa na mtoa huduma wenu, msiache kujitokeza na kisha mlalamike uamuzi unapokuwa umetolewa.”



Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu, akiwa kwenye mazungumzo na ujumbe wa wawekezaji kutoka... waliokuwa nchini hivi karibuni kuangalia mazingira ya uwekezaji. Mkutano wa Afur utatoa fursa kwa Tanzania kujitangaza zaidi kwa wawekezaji kama hawa.

EWURA na SUMATRA wawa wenyeji wa mkutano wa AFUR

Na Mwandishi wetu

MAMLAKA ya Uchibiti wa Nishati na Maji (EWURA) na ile ya Uchibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) zilikuwa wenyeji wa Mkutano Mkuu wa 10 wa Mwaka wa Vyombo vya Uchibiti wa Huduma Afrika (AFUR) uliofanyika jijini Arusha mwezi Aprili mwaka huu.

AFUR ni mpango ulioanzishwa na Ushirikiano Mpya wa Maendeleo kwa Afrika (NEPAD). Iliizinduliwa rasmi Novemba 2002 kama chombo cha kujitolea cha Wadhibiti wa Huduma wa Afrika kikiwa na Katiba yake.

Umjoja huo unalenga kuanzisha na kuendeleza ushirikiano miongoni mwa wadhibiti wa huduma wa kitafrika ili kuchangia ukuaji na maendeleo ya kiuchumi na kijamii wa bara hilo. Lengo la msingi la AFUR ni juu ya masuala yanayohusiana na usimamizi wa miundombinu ya sekta za mawasiliano, nishati, usafirishaji, maji na usafi. Kwa miaka kadhaa sasa, AFUR imekuwa chombo ambako wadhibiti wa huduma Afrika wanakutana kuanadaa

na kuharakisha mikakati ya maendeleo ya mpango wa udhibiti kwa kiwango huduma na kuwezesha kutoa bei nzuri na kuleta maendeleo na ushirikiano baina ya miundombinu barani Afrika.

“Huu ni mkutano wa kimataifa ambao uliwakutanisha washiriki wapatao 200 kutoka taasisi za kutoa huduma za nishati, kampuni za usafirishaji, benki za uwekezaji, kampuni za ushauri na wadau wengine ili kukutana na maofisa wa ngazi za juu wa wakala za udhibiti katika umeme, gesi asilia, maji na usafi, usafiri na mawasiliano, bandari na melli; wawekezaji, huduma, serikali na mashirika ya kimataifa kutoka Afrika na sehemu zingine duniani,” alisema Bw. Felix Ngamtagosi, Mwenyekiti wa Kamati Mwenyeji ya Maandalizi ya AFUR na ambaye pia ni Mkurugenzi wa Uchumi EWURA.

Mkutano wa mwaka huu ulikuwa chini ya kaulimbiu ya “Changamoto za Uwazi: Uhusiano kati ya Wadhibiti na Wadau”

Bw. Ngamtagosi alisema kutokana na uzito wa masuala mbalimbali yaliyojadiliwa, na idadi ya washiriki, Tanzania ilipata nafasi kubwa ya kutungua fursa zake za uwekezaji kwa dunia. Mkutano wa mwaka huu ulikuwa chini ya kaulimbiu ya “Changamoto za Uwazi: Uhusiano kati ya Wadhibiti na Wadau”, alisema.

Aliongeza kuwa mkutano huo ulitoa fursa muhimu ya kupata soko la bidhaa kwa ajili ya kundi muhimu la watu, na pia kuzisaidia EWURA na SUMATRA katika azma yao ya kuimarisha shughuli zao za udhibiti nchini Tanzania kwa kuongeza welewa na kujenga mitandao na wataalamu wengine, bila kutaja manufaa mengine zaidi ambayo ni pamoja na kutangaza vivutio vingine vya asili ambavyo nchi inavyo, pamoja na huduma na bidhaa zinazoweza kutumiwa na washiriki wa mkutano huo.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw. Haruna Masebu, ndiye Mwenyekiti wa sasa wa AFUR baada ya kuchaguliwa kwa kauli moja mapema mwaka huu. Atakuwa madarakani kwa miaka mitatu ilayo. Mapendekezo ya uteuzi wa Masebu yaliwasilishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Umeme ya Cameroon (ARSEL) na kuungwa mkono na zaidi ya wanachama 20 wa AFUR waliohudhuria mkutano wa chombo hicho Afrika Kusini. Uchaguzi huo ulikuwa wa aina yake ambao haukufanyika kupitia sanduku la kura kama ilivyo kawaida, kwa kuwa wajumbe wote kwa kauli moja waliimchagua Bw. Masebu katika Mkutano Mkuu wa Tisa wa Mwaka.

asilimia 49. Matuta ya taa yalitumika lita 650,000 kwa mwaka, lakini uhalisia ni kwamba nchi inatumia lita 200,000 sawa na pungufu ya asilimia 30.77. Mtu anaweza kujiliza mengine yalikuwa yakienda wapi ... uchakachuai!

Kampuni hizo zimetakiwa kueleza ni kwa nini hatua za kinidhamu, ikiwa ni pamoja na kufutiwa leseni zao, zisichukuliwe na Mdhidhi kwa sababu wameshindwa kufanya biashara kulingana na leseni walizonazo.

Hivyo, utambuzi wa matumizi hayo halisi yanayofanya asilimia 50 pia umesababisha ongezeko la kodii inayokusanywa, ambayo vinginevyo ilikuwa ikiishia katika mifuko isiyojulikana.

Hali kadhalika, BPS imewzesha kubaini kiwango halisi cha hasara baharini ambayo kwa kawaida hutokea pale matuta yanaposafirishwa kati ya bandari kadhaa.

Ambapo kabla ya BPS kilichokuwa kikifanyika kilikuwa ni kutathmini, sasa BPS imewzesha kupatikana kwa takwimu sahihi ambazo zinakokotolewa na kupata hasara ya baharini.



Kuficha matuta huku soko likiwa na uhitaji mkubwa ni ukikwaji wa masharti ya biashara ya matuta ambao huweza kuadhibiwa vikali.

Waagizaji mafuta kukabiliwa na shoka la Mdhibiti

Na Mwandishi wetu

TAKRIBAN waagizaji 16 wa bidhaa za petroli wamepelekewa agizo la kuwataka waeleze ni kwa nini wasitufiwe leseni zao kwa kushindwa kuagiza mafuta kwa miezi sita mfululizo.

Kushindwa kwa kampuni hizo kuagiza mazao ya mafuta ya petroli kwa mujibu wa leseni zao ni kinyume cha masharti ya leseni ambayo yanawataka kuanza biashara hiyo mara tu wanapopata leseni kutoka kwa Mdhibiti.

“Kwa kweli, kampuni hizo zimetakiwa kueleza ni kwa nini hata za kinidhamu, ikiwa ni pamoja na kufutiwa leseni zao, zisichukuliwe na Mdhibiti kwa sababu wameshindwa kufanya biashara kulingana na leseni walizonazo,” alisema Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo.

Kampuni hizo 16 ni pamoja na Tanga Petroleum Co. Ltd, DFCG International Ltd, Mohammed Twalib Petro Station Ltd, Petro (T) Ltd, Amazon Petroleum, Danvic Petroleum, na Petro Sol (T) Ltd.

Nyingine ni Bright Star Energy Co. Ltd, EXCO Oil Co. Ltd, Petromark Africa, Oil Link (T), Riva Oils (T) Ltd, Metrol Petroleum (T) Ltd, Afroil Investment Ltd, COPEC na Swiss Singapore Oversees Ltd.

Ili kuondokana na hali hiyo, Mdhibiti aliiitisha mkutano wa dharura na wadau, ikiwa ni pamoja na kampuni za kuza mafuta na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambako ilikubalika kwamba mtoza kodi aruhusu asilimia 50 ya mafuta yanayopita nchini ambayo yanazuiwa yaingie soko la ndani baada ya kodi kulipwa na wanunuzi.

Hata hivyo, hata baada ya makubaliano hayo na kampuni hizo zinazouza mafuta ili kusaidia biashara kwenda sawa, baadhi yao waliendelea kuhodhi mafuta hayo. Mathalan kampuni ya Puma Energy (T) Ltd ina lita milioni 23 kwenye akiba yake, na ilitakiwa ijieleze kwa nini ina kiasi hicho cha

akiba wakati soko likikosa mafuta. Kampuni nyingine, Kobil Tanzania Limited, ilitakiwa kueleza ni kwa nini haijauza mafuta kwa wafanyabiashara wa rejareja, hata ambayo ni dhahiri ni tabia ya kibaguzi sokoni.

Wakati huo huo, EWURA imeitaka kampuni tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), COPEC, ambayo mwaka jana ilipewa leseni ya kuagiza mafuta ya akiba kuanza biashara hiyo.

Mkakati huo wa kuwa na akiba ya mafuta utahakikisha kwamba nchi haipati mataizo ya mafuta wakati wote, hata nyakati za dharura na mazingira mengine yasiyotarajiwa. Hata hivyo, kwa kuanza Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja (BPS), baada ya miaka miwili na nusu ya mjadala mkali juu ya kama Tanzania inapaswa kutumia mfumo huo au la, kuna hisia za jumla, kwamba baadhi ya wadau wangependa kuona mfumo huo unasitishwa.

Kwa sababu hii, kumekuwa na kampeni za kimya ili kupinga mfumo huo wa BPS, ikisema umeshindwa kuleta matokeo yaliyotarajiwa.

Juhudi ambazo zinalinga kuhujumu mfumo huo, haziangalii manufaa yaliyopatikana kutokana na BPS mpaka sasa, kama vile kutambua kiasi halisi cha mafuta ambayo nchi inaagiza na kutumia, ambapo pia inawezesha kubaini kodi iliyolipwa.

Mathalan, kabla ya BPS, takwimu zilionesha kwamba Tanzania ilitumia lita 875,000 kwa mwaka, lakini baada ya BPS kuanza, ilibainika kwamba matumizi ya mwaka yalikuwa lita 1,700,000, ambalo ni ongezeko la asilimia 50.

Kwa matumizi ya dizeli, kabla ya BPS ilisemekana kuwa lita 1,700,000 kwa mwaka, lakini zikapanda hadi 3,540,000 baada ya mfumo huo kuanza, sawa na ongezeko la



Mkurugenzi wa Udhidi wa Kiuchumi wa EWURA, Bw. Felix Ngamagosi akiwasilisha mada juu ya matakwa ya kisheria kuitanya EWURA idhibiti bei na tozo kwenye sekta ya nishati kwenye Mkutano wa taffishi iliohusu TANESCO kupandisha bei ya umeme, Disemba 2012, Dar es Salaam.

wa mtumo huo. RSM imeegemea katika kanuni ambazo zimetajwa katika hoja za kisheria, kisera, kiuchumi na kiutendaji, vyote vikilenga katika kuwa na bei ambazo zinaakisi gharama. Hii inamaanisha kwamba RSM hiyo imeundwa ili kuhusisha gharama zote halali kwa vitengo gharama bila kuhusisha ruzuku yoyote.

Mdhibiti kutumia njia mpya za kufahamu gharama za umeme

Na Mwandishi wetu

MAMLAKA ya Udhidi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imekuja na njia mpya ambazo zitasaidia kufikia gharama za kutoa huduma ya umeme Tanzania.

Bei zilizopendekezwa chini ya Utaratibu wa Kupanga Viwango (RSM) kwa ajili ya sekta ya umeme Tanzania Bara na Utati wa Gharama za Huduma (COSS) kwa ajili ya TANESCO, ni hatua kubwa kuelekea kufikia kuwa na bei halisi ya matumizi kwa sekta ya umeme Tanzania.

Mwaka 2011, Mamlaka ilikubaliana na mshauri huru, AF-MERCADOS wa Hispania, ili kutekeleza majukumu hayo, ambayo yatakuwa mapinduzi kwa jinsi Mdhibiti anavyoshughulikia maombi ya bei.

"Kanuni zilizozanzishwa juu ya utaratibu mpya ni msingi bora wa kuamua gharama za kutoa huduma za umeme kwa TANESCO," anasema Mkurugenzi wa Uchumi wa EWURA, Bw. Felix Ngamlagosi.

usambazaji wa nishati hiyo.

Kwa mujibu wa Bw. Ngamlagosi, wastani wa bei ya rejareja utaongeza bei ya utaji, ugavi na usambazaji. Tangu iundwe mwaka 2006, EWURA imeanzisha vyombo vya udhibiti ambavyo

vinafasiri sera, kanuni na taratibu za udhibiti. Ni vema kuelezea, kwamba Mamlaka iliandaa Miongozo ya Maombi ya Bei mwaka 2006 ambayo iliboresha mwaka 2009

"Kanuni zilizozanzishwa juu ya utaratibu mpya ni msingi bora wa kuamua gharama za kutoa huduma za umeme kwa TANESCO"

na kuwa Miongozo ya Maombi ya Bei ya mwaka 2009. Miongozo hiyo miwili inaeleza kanuni na mahitaji ya taarifa ambazo waombaaji wanapaswa kuwasilisha kwenye Mamlaka wanapokuwa wanajaza maombi yao. Taarifa hiyo inahusisha taarifa za mwisho, taarifa za uendeshaaji za mwaka, mahesabu ya fedha yaliyokaguliwa na mpango kazi.

Miongozo hiyo pia inatoa taratibu kwamba Mamlaka itafuatilia wakati inatathmini maombi, ikiwa ni pamoja na kuendesha uchunguzi.

Mamlaka inalenga kupata utaratibu mzuri wa kimataifa katika usimamizi wa udhibiti kwa kuboresha ubashiri, msimamo na uwazi katika mchakato wa kufikia utoaji uamuzi.

Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 ni zana kuu ya kisheria katika sekta ya umeme, na wakati wa mgogoro, vyombo vingine hupewa kipaumbele (mathalan Sheria ya EWURA).

Sheria hiyo inaweka vipengere muhimu vya mpango wa udhibiti na mahitaji kadhaa kuhusu kupanga bei. Nguvu za kupanga bei za Mamlaka zimeainishwa katika kifungu 5(b) cha sheria hiyo, ambacho kinaitaka Mamlaka kuidhinisha na kutekeleza bei na ada zinazotolewa na wafanyabiashara.

Tangu kifungu namba 8(1) cha Sheria hiyo kijumuishhe wafanyabiashara hao katika utaji, ugavi na usambazaji na mfumo unaendesha shughuli hizo, hii inamaanisha kwamba Mamlaka inahitajika kuamua bei kwa ajili ya, pamoja na mambo mengine, vipengere vya uuzaaji wa jumla, ugavi na usambazaji.

Ubainisho wa gharama za utaji na usambazaji na bei vimeegemea katika Mpango Mkuu wa Mfumo wa Umeme ambao unaonesha mipango iliyopo na ijayo ya upanuzi

Kwa sababu hii, kiasi cha hasara iliyolipwa ambayo ilikuwa katika fomula ya upangaji bei, imepungua kwa kiwango kikubwa. Pale ambapo malipo yalilikadiriwa kuwa kati ya asilimia 0.25 hadi asilimia 0.5, hivi sasa kiwango cha hasara hii ni 0.0 kwa baadhi ya bidhaa zinazoagizwa.

Paliipokuwa na ugonvu wa kukokotoa na kukusanya takwimu muhimu na sahihi enzi za uagizaji wa kampuni moja moja, chini ya BPS, imedhihirika kuwa kama nchi, Tanzania inaweza kupata takwimu sahihi kuhusu masuala yanayohusiana na matuta-kutoka uagizaji wa matuta kwa ajili ya matumizi ya siku na hivyo kurahisisha mipango ya kibajeti na uendeshaaji.

Chini ya BPS, hivi sasa inawezekana kukokotoa gharama za shehena tangu ikiwa baharini hadi kupanga bei ya mwisho, ambapo kabla ya mtumo wa sasa kazi hii ilikuwa inafanyika kwa makadirio. Haiwezekani pia sasa kwa kampuni za matuta za kigeni kuendana na bei inayopangwa nchini kwao, kwa misingi ya matuta yanayoangizwa kutoka nchi zao, hivyo kuathiri upangaji huo.

Hali inaonesha kushuka kwa ada hizo, na pia ongezeko la ushiriki wa kampuni zilizoonesha nia ya kuomba zabuni. Jambo kubwa ni kupungua kwa idadi ya siku za meli kusubiri kupakua mzigo hasa kunapokuwa na meli nyingi, hivyo kuvutia kile kinachojulikana kama fidia za ucheleweshaji mizigo ambazo zinatozwa dola 20,000 za Marekani kwa siku.

Hali inaonesha kushuka kwa ada hizo, na pia ongezeko la ushiriki wa kampuni zilizoonesha nia ya kuomba zabuni.

Jambo kubwa ni kupungua kwa idadi ya siku za meli kusubiri kupakua mzigo hasa kunapokuwa na meli nyingi, hivyo kuvutia kile kinachojulikana kama fidia za ucheleweshaji mizigo ambazo zinatozwa dola 20,000 za Marekani kwa siku. Hata hivyo, baadhi ya shehena katika zabuni ya tatu meli zao zilika muda mrefu na hivyo kusababisha kutozwa faini, hasa ni kwa sababu wamiliki wao waliagiza shehena kubwa ya matuta kuliko mahitaji yao halisi, hivyo kusababisha kupungua kwa kasi ya upakuaji. Hata hivyo, hali hii sasa ni zuri kuliko zamani.

Kuanza kwa SPM Novemba 2012 kumeshuhudia ongezeko la uwezo wa Tanzania kuhudumia meli kubwa zaidi za matuta hadi tani za ujazo 120,000, hali ambayo inaionyesha pia katika kuboreka kwa biashara ya matuta. Hali kadhalika, kwa kuwa na mtumo wa BPS, ni rahisi sasa kubaini hasara zinazopakana katika usafirishaji matuta baharini kupitia takwimu sahihi zilizotolewa na mkaguzi wa huduma za majini aliyependekewa na pande zote mbili.

Mwaka mmoja wa BPS: Punguzo la fidia, takwimu za uhakika



Meli ya MT. Alpine, ikipakua shehena ya mafuta Kurasini. Ilikuwa moja ya meli za kwanza kubwa kushusha shehena ya mafuta chini ya Mfumo wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja.

Na Mwandishi wetu

Ni mwaka mmoja sasa tangu nchi ilipoanzisha Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja (BPS). Mfumo huo, ambao kuanzishwa kwa kuliikabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa baadhi ya wadau wenye nguvu na ushawishi mkubwa, umeshuhudia sekta ya mafuta ikipata mafanikio ambayo pia yamesaidia kuimarisha uchumi wa nchi.

Muda mrefu, upandaji holela na wa kasi wa bei ya mafuta utadhibitiwa kwa kipindi kirefu kijacho.

Kufikia Januari 2013, takriban zabuni nane zilikuwa zimefunguliwa. Kampuni mbili za kimataifa za AUGUSTA Energy SA na ADDAX Energy zilikuwa zimeshinda zabuni tatu kila moja. La muhimu zaidi ni kwamba kwa mara ya kwanza katika historia ya BPS nchini, kampuni ya ndani ya Gapco imeshinda zabuni katika mchuano mkali na kampuni zingine za kimataifa. Ada za kuanzia kati ya juu ya 59.27 na 42.98, zimekuwa na athari chanya katika zabuni hizo za kiushindani.

TANESCO yaondoa maombi ya kurekebisha bei za umeme



Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw. Felchessmi Mramba, akitetea maombi ya shirika lake kutaka bei ya umeme ipande wakati wa mkutano wa tafitishi uliofanyika Dar es Salaam hivi karibuni. Hata hivyo, shirika hilo lilifuta maombi yake hayo.

Na Mwandishi wetu

Shirika la Umeme Tanzania limeondoa maombi yake ya kurekebisha bei za umeme yaliyokuwa yakishughulikiwa na Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA.) Kuondoa kwa maombi hayo kuna maana kuwa hakutakuwa na ongezeko la bei ya umeme kwa wateja, waliu kwa sasa. Maombi hayo ya kurekebisha bei za umeme yaliianzia Novemba 2011, ambapo TANESCO iliomba kwa dharura kupandisha bei za umeme kwa wastani wa asilimia 155 kwa wateja wote, hata ambayo ingeanza rasmi Januari 2012.

Hata hivyo, kabla ya kufikia mwisho wa mchakato wa marekebisho ya bei, TANESCO kupitia barua yake ya tarehe 14 Januari 2013, ilifuta maombi hayo na kuomba viwango vya bei vinavyotumika sasa viweze kuelekea. Kufuatia maombi hayo, Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA iliamua manamo Januari 14, 2013, kufuta agizo lake la marekebisho ya dharura ya viwango vya bei za umeme za TANESCO, wakati huo huo ikiridhiana viwango vya sasa viendelee kutumika.

na kushauri namna bora ya kuweka viwango vya umeme Tanzania (RSM), na gharama za uzalishaji na usambazaji umemewa TANESCO (COSS), viwango vilivyopendekewa vilikuwa asilimia 33.8 kwa mwaka 2013; 0.85 kwa 2014 na 15.14 kwa 2015. EWURA ilifanya mchakato wa kukusanya maoni ya wadau kati ya Disemba 2012 na Januari 2013, ili kujiridhisha na sababu za mapendekazo hayo ya kupanda kwa bei kwa Tanesco, kwa mujibu wa sheria kipingele 19(2)(b) cha sheria ya EWURA.

Kutoka Dawati la Mkurugenzi Mkuu



Bw. Haruna Masebu

Mpendwa msomaji,
katika harakati za kuanza mwaka 2013, ningependa kuchukua fursa hii kwa kumtaka kila mtu Heri ya Mwaka Mpya wenye furaha tele, na pia nagependa kutoa shukrani za dhati kwa baraka za kuwa na uwezo wa kushuhudia Mwaka huu mpya.

Kama mnavyofahamu, EWURA inajitahidi kuimarisha ubora wa huduma katika sekta zinazodhibitiwa, yaani Umeme, Mafuta, gesi asilia na Maji, kwa faida ya jamii ya Watanzania, kwa kuzingatia taratibu za kimataifa za udhibiti bora (*International Best Practices*). Taratibu hizo huelezea msingi wa udhibiti bora, kwa maana ya umuhimu wa kuwa mdhibiti mwenye uhuru, uwazi, uwajibikaji na uadilifu. Tangu kuanzishwa kwake, EWURA imeendelea kutekeleza ahadi yake ya kufuata viwango vya kimataifa kwa kupitia mchakato wenye kueleweka, uwazi na kushauriana.

Jarida la EWURA lina makala zinazozingatia masuala yanayohusiana na sekta zinazodhibitiwa. Ni furaha yangu kwa mara nyingine tena kuwakaribisha kusoma makala zilizomo katika jarida hili, ambalo lipo katika toleo lake la nane, kwa lengo la kukua ufahamu juu ya masuala yanayohusiana na sekta zinazodhibitiwa.

Ndugu msomaji, kama mjuavyo, 2012 ulikuwa mwaka mguumu kidogo kwa EWURA, kwa kuwa mamlaka ilishughulikia masuala yanayohusiana na mfuomo wa *Bulk Procurement System* (BPS) ama uagizaji wa mafuta kwa pamoja, katika sekta ya mafuta ya petroli na kukamilika kwa *Cost of Service Study* (COSS) ama Utafiti wa Gharama za Kuzalisha Umeme, kwa kutaja mifano michache, sekta zote mbili zikiwa zenye maslahi ya juu katika usalama wa taifa.

EWURA pia ilihusika katika maandazi ya sheria na sera ya nchi ya gesi asilia (*Natural Gas Policy*).

Aidha, mwaka 2012 kulikuwa na mataniko muhimu kwa jamii ya Kitanzania kutokana na uadilifu wa kazi wa EWURA katika sekta zilizodhibitiwa. Kwa mifano, watoa huduma katika sekta ya umeme waliendelea kutekeleza mambo mbali yaliyoagizwa na ama Mdhibiti ama wateja wao, wakati wawekezaji waliendelea kuwa na imani zaidi, kwamba vitega uchumi vyao vitakuwa salama hapa Tanzania, kutokana na mazingira ya kirafiki kwa wawekezaji. Katika sekta ya mafuta ya petroli, mfuomo wa BPS uliwezesha usambazaji wa bidhaa za mafuta ya petroli kuingia nchini kwa pamoja, wakati huo, mpango wa uwekaji vinasaba kwenye mafuta (*Fuel Marking Program*) ukiendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza uchakachaji wa mafuta na wizi wa mafuta ya soko la nje yasiyolipwa kodi (transit fuel dumping). Maendeleo katika sekta ya maji ni pamoja na upanuzi wa mtandao wa ugavi wa maji, kuongezeka kwa idadi ya wateja waliotungwa mita za maji (*metering ratio*), uzalishaji maji na idadi ya wateja kwa ujumla; na kupunguza upotevu wa maji.

EWURA itaendelea kuzingatia viwango vya kimataifa na utamaduni wa udhibiti bora. Tutaendelea kushiriki katika masuala ya kimataifa kwa kupitia mashirika mbalimbali ya kiudhibiti kwa nia ya kukua maadili haya. EWURA pia itadumisha jukumu lake katika maandazi ya sheria na sera ya nchi ya gesi asilia ili kuhakikisha kwamba sekta ya maji ni kwa faida ya wote. Hatimaye, napenda kuwashukuru wadau wote kwa ushirikiano wao katika shughuli za kila siku ya Mamlaka.

Tafadhali ungana na mimi katika kusoma makala zinazopatikana katika jarida hili la EWURA.

Wataka wa Mhavi

WAPENZI wasomaji, ninayo furaha kuwakaribisha tena katika toleo letu la Jarida la Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Hili ni toleo la nane, ambalo pia ni moja ya vyombo vingi vilivyoanzishwa na Mamlaka kwa lengo la kutoa maarifa, uelewa na elimu kwa umma juu ya sekta za huduma na zilizochini ya Mamlaka hii.

Kupitia Jarida hili la EWURA, watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA wameweza kupata maarifa juu ya haki na wajibu wao. Pia limeweza kuwapa waliaji mwanga wa jinsi malalamiko na migogoro inavyoweza kuanzishwa na kutatuliwa.

Ni matumaini yetu, kwamba toleo hili la nane litaimarisha maarifa zaidi, uelewa zaidi na elimu zaidi juu ya masuala ya udhibiti na hivyo kuwa miongoni mwa zana bora zaidi kwa ajili ya kampeni kwa umma, ambazo zimeanzishwa na Mamlaka.

Matleo mengi ya Jarida la EWURA ambayo huchapishwa kwa kiswahili na Kiingereza, yameiweka Mamlaka katika kiwango cha juu katika kujiunga umma imani.

Mamlaka imeshuhudia ongezeko la malalamiko juu ya sekta za petroli, umeme na maji ambayo yametoa miongoni mwa mambo mengine mchango wa Jarida la EWURA juu ya uanzishwaji wa elimu kwa umma ambayo imewafanya waliaji kujua haki na wajibu wao.

Katika toleo hili la nane, wasomaji mtaendelea kupata maarifa na uelewa kwa kusoma makala kadhaa za kuvutia kutoka sekta zetu ambazo zinadhhibitiwa na Mamlaka.

Karibuni!



Bw. Titus Kaguo

Waraka wa Mhariri.....	3
Kutoka Dawati la Mkurugenzi Mkuu.....	4
TANESCO yaondoa maombi ya kurekebisha bei za umeme.....	5
Mwaka mmoja wa BPS: Punguzo la fidia, takwimu za uhakika	6
Mdhibiti kutumia njia mpya za kufahamu gharama za umeme.....	8
Waagizaji mafuta kukabiliwa na shoka la Mdhibiti.....	10
EWURA na SUMATRA wawa wenyeji wa mkutano wa AFUR.....	12
Jitokezeni kutoa maoni badala ya kulalamika - Mkuu wa Mkoa Dar	14
Waomba leseni kuzalisha umeme wa megawati 150.....	16
Habari katika picha	18

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw. Felchesmi Miramba, akitetea maombi ya shirika lake kutaka bei ya umeme ipande, wakati wa mkutano wa tatiishi uliofanyika Dar es Salaam hivi karibuni. Hata hivyo, shirika hilo lilituta maombi yake hayo.



TANESCO YAONDOA MAOMBI YA KUREKEBISHA BEI ZA UMEME

ISSN 1821 - 7273 TOLEO NA. 008

MEI 2013

Newsletter

Energy and Water Utilities Regulatory Authority



HALI UZWI